**SEKTA YA NISHATI (TANESCO)**

Tanesco Wilaya ya Ileje inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali katika vijiji na mitaa kwa kutumia bajeti ya **TANESCO** pamoja na miradi inayofadhiliwa na **REA** kwa mchanganuo ufuatao.

**Miradi inayofanywa kwa gharama za Tanesco ni kama ifutavyo**
Tuna jumla ya miradi 15 inayofanywa na Tanesco katika sehemu mbali mbali katika wilaya yetu ya ileje miradi hiyo ni Uboreshaji wa voltage(voltage improvement) na Uunganishaji upya (Custormer captuaring)

**Kuunganisha huduma ya umeme kwa wateja kuanzia Julai 2022 hadi Desemba 2022**
Wateja wa njia moja (1Q)=590 **na** Wateja wa njia tatu (3Q)=21**Jumla ya wateja ni 611**
Malengo yalikuwa ni kuunganishia jumla ya wateja 300 Kwa kipindi hicho Ni ongezeko la zaidi ya 100% hivyo, malengo yamefikiwa na kuzidi, hii ni kutokana na upatikanaji wa vifaa kwa wakati na huduma ya NICONECT.

**Miradi inayotekelezwa kutokana na bajeti ya rea;**
Usambazaji wa umeme katika Wilaya ya Ileje umeendelea katika kata na vijiji mbalimbali kupitia REA AWAMU YA TATU MZUNGUKO WA PILI kama ifuatavyo;
**Jedwali namba 5**

| | **IDADI** | **ZENYE/VYENYE UMEME** | **ZISIZO/VISIVYO NA UMEME** | **MPANGO WA KUPELEKA UMEME** |
|---|---|---|---|---|
| Kata | 18 | 18 | 0 | Kata zote zina umeme |
| Vijiji | 71 | 53 | 18 | REA III-II |
| Vitongoji | 316 | 104 | 212 | Densification |

Vijiji 22 ambavyo havina umeme mpango wa kuvipeleka umeme umeshakamilika na mkandarasi yuko saiti kwa hatua mbalimbali. Ilikuwa mkandarasi ajenge kilomita 1 kwenye kila kijiji ila kwa sasa mkandarasi ameambiwa ajenge kilometa tatu kwenye kila kijiji na amesha maliza hatua ya survey ili aanze kuleta material kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hizo kilometa zilizo ongezeka.

**Jedwali lifuatalo linaonyesha maendeleo ya mradi wa rea iii round ii hadi kufikia Desemba 2022.**
Kwa hatua za awali, survey ilishakamilika kwa vijiji vyote 22, na sasa mradi uko katika hatua mbalimbali kwa vijiji 22 ifuatavyo;

**MAENDELEO YA MRADI WA REA 3 ROUND 2 ILEJE**

**Jedwali namba 7**

| **S/N** | **WILAYA** | **KIJIJI** | **KAZI ILIYOFANYIKA** | **WIGO WA KAZI** | **WIGO ULIOFANYIKA** | **ASILIMIA YA KAZI HUSIKA** |
|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | | | ILIYOFANYIKA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MV (KM) | LV (KM) | MV (KM) | LV (KM) | MV (KM) | LV (KM) |
| 1 | ILEJE | SHUBA | Kusimamisha nguzo | 4 | 1 | 4 | 0 | 100 | 0 |
| 2 | ILEJE | MBEMBATI | Kusimamisha nguzo | 5 | 1 | 5 | 0 | 100 | 0 |
| 3 | ILEJE | ITEGA | Kusimamisha nguzo | 7 | 1 | 6 | 0 | 100 | 100 |
| 4 | ILEJE | MBANGALA | Kuvuta waya | 3 | 1 | 3 | 1 | 75 | 0 |
| 5 | ILEJE | SHIRINGA | Kusimamisha nguzo | 3 | 1 | 1 | 1 | 100 | 100 |
| 6 | ILEJE | CHIBILA | Kusimamisha nguzo | 2 | 1 | 1 | 1 | 70 | 55 |
| 7 | ILEJE | IBANDI | Kufunga mita | 3 | 1 | 3 | 1 | 100 | 100 |
| 8 | ILEJE | NDAPWA | Kusimamisha nguzo | 0.6 | 1 | 0.6 | 1 | 100 | 100 |
| 9 | ILEJE | BULANGA | Kufunga mita | 1.4 | 1 | 1.4 | 1 | 100 | 100 |
| 10 | ILEJE | IBETA | Kuvuta waya | 1.7 | 1 | 1.7 | 0 | 100 | 100 |
| 11 | ILEJE | BWIPA | Kuunga wateja | 0.02 | 1 | 0.02 | 1 | 100 | 100 |
| 12 | ILEJE | SHEYO | Kusimamisha nguzo | - | 1 | - | 0 | - | 100 |
| 13 | ILEJE | CHIKUMBULU | Kusimamisha nguzo | 6.8 | 1 | 2.5 | 0 | 80 | 0 |
| 14 | ILEJE | MAKOGA | Kusimamisha nguzo | 1.7 | 1 | 1.7 | 0 | 100 | 100 |
| 15 | ILEJE | KISYESYE | Kusimamisha nguzo | 4 | 1 | 2 | 0 | 100 | 0 |
| 16 | ILEJE | BUFULA | Kuchimba mashimo | 2.1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 17 | ILEJE | SHINJI | Kusimasha nguzo | 6.5 | 1 | 6.5 | 1 | 100 | 100 |
| 18 | ILEJE | YENZEBWE | Kusimamisha nguzo | 5.4 | 1 | 5.4 | 0 | 95 | 100 |
| 19 | ILEJE | IBEZYA | Kuchimba mashimo | 5.1 | 1 | 5.1 | 1 | 100 | 100 |
| 20 | ILEJE | CHITETE | Kuvuta waya | 2.5 | 1 | 2.5 | 0 | 95 | 100 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 21 | ILEJE | MABULA | Kusimamisha nguzo | 3.5 | 1 | 2.5 | 0 | 90 | 100 |
| 22 | ILEJE | IWALA | Kuchimba mashimo | 0.8 | 1 | 0.4 | 0 | 50 | 0 |

Ilitakiwa Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Desemba,2022, tulitarajia kuwasha vijiji 8 vya Ibandi, Bwipa, Bulanga ,Ibeta,Shinji,Makoga,Shiringa, na Ndapwa. Mkandarasi ameanza kufunga mita na wananchi wa bwipa na bulanga wameshafungiwa mita na umeme unawaka sasa,wananchi wa ibeta na ibandi wameshalipia tayali kwa kufungiwa mita na mpaka tarehe ya leo jumla ya wateja 35 wamefungiwa umeme

**Changamoto**

Upatikanaji hafifu wa vifaa vya kazi kwa wakati vinavyowawezesha wataalamu kukamilisha kazi na Ukosefu wa usafiri wa gari kwa ajili ya kufuatilia miradi hiyo kwa wakati.

**SEKTA YA VIWANDA.**

Wilaya ya Ileje inatekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 – 2022/23 ambao unalenga Kujenga Uchumi wa Viwanda ilikuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu. Lengo kuu ni kuongeza kasi ya kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 inayoitaka Tanzania kuwa Nchi yenye Uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025. Ili kufikia lengo hili yanahitajika mageuzi ya kifikra na kimtazamo katika jamii yetu. Aidha, Serikali ya Mkoa imeweka malengo ya kujenga viwanda 100 ifikapo mwaka 2022/23, viwanda 20 kila Wilaya. Katika kutekeleza hili Wilaya ya Ileje imefanikiwa kutenga Ekari 10,407.5 katika Kata 18 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa. Wilaya pia imewashirikisha Wadau mbalimbali katika sekta binafsi kwa kupitia Ubia (PPP).

Wilaya ya Ileje ina fursa mbalimbali za uwekezaji wa Viwanda kama vile Maporomoko ya maji yaliyopo kijiji cha Bwenda kata ya Lubanda, Maporomoko ya maji yaliyopo kijiji cha Lusalala kata ya Sange, Makaa ya Mawe; Mifugo aina ya Ng'ombe, Mbuzi, Nguruwe na Kuku. Kilimo kama Kahawa, iriki, karanga, Mahindi na usafirishaji wa mahindi, karanga na mbao.

**SEKTA YA BIASHARA**

Mbali na Kilimo, wananchi wa Wilaya ya Ileje hujishughulisha pia na biashara ambayo vilevile kwa sehemu kubwa hutegemea kilimo. Aidha, baadhi ya wananchi hujishughulisha na biashara ya maduka ya rejareja,shule za watu binafsi (msingi na sekondari),Kuuza vifaa vya ujenzi,Kuuza mbao,Kuuza vifaa vya maofisini,Mashine za kusaga na kukoboa nafaka,Butcher, Saluni za kike na za kiume,Kuuza vifaa vya pikipiki, vifaa vya magari na baiskeli, Uuzaji wa pembejeo za Kilimo na mifugo, Migahawa, Vituo vya mafuta ya petrol,Kuuza dawa muhimu za binadamu,Mawakala wa huduma za kifedha, nyumba za kulala wageni, Kusafirisha abiria na mizigo kutoka ndani ya wilaya

kwenda nje ya wilaya, mkoa au nje ya nchi. Hali ya biashara ni ya kuridhisha. Bidhaa muhimu zinapatikana kwa bei ya kawaida.

**Hali ya Masoko ya Mazao ya Biashara na Chakula**

Katika kukuza na kuendeleza sekta ya Viwanda, biashara na Masoko Wilaya imekuwa ikitekeleza shughuli mbalimbali kama:

- Kuimarisha Baraza la Biashara la Wilaya ya Ileje.
- Kuendelea kutoa elimu ya biashara kwa wadau mbalimbali vikiwemo vikundi vya wakulima ambao wamekuwa wakipata elimu ya usindikaji mazao ya chakula kwa lengo la kuongeza thamani na ubora wabidhaa.
- Wilaya inajumla ya viwanda vidogo 493 vinavyojishughulisha na shughuli mbalimbali kama: Kukoboa na kusaga nafaka (218), Kukamua alizeti (7), Kuchomelea vyuma (23), Fundi seremala (106), Fundi cherehani (81), Kupasua mbao (51), Wahunzi (6), Kukoboa mpunga (1).

**Idadi ya leseni zilizotolewa kwa mwaka 2022/2023**

Kwa mujibu wa sheria ya leseni za biashara namba 25 ya mwaka 1972 kila biashara yenye eneo la kudumu (Premise) inapaswa kuwa na leseni ya biashara na kiwango kwa kila biashara imewekwa kwenye Finance Act ya mwaka 2014. Kuanzia tarehe 1/7/2022 hadi sasa (14/1/2023) Jumla ya leseni zilizotolewa ni 210 kwa mchanganuo ufuatao: Pembejeo za Kilimo na Mifugo (Agrovet) 3; Butcher 1; Duka la dawa muhimu 7; Duka la Rejareja 58; Environmental Consultants 1; Fundi seremala 1; Fundi ujenzi 1; Kuchomelea 2; Kununua na kuuza nafaka 7; Kuuza CD 1; Kuuza Computer na Vifaa vyake 1; Kuuza Gesi 1; Kuuza magodoro 2; Kuuza mbao 4; Kuuza mbolea 12; Kuuza nguo za mtumba 3; Kuuza samaki 1; Kuuza simu 1; Kuuza solar 1; Kuuza vinywaji 2; Kuuza vyombo 1; Mashine ya kukamua alizeti 3; Mashine ya kukoboa na kusaga nafaka 21; Mashine ya kuranda mbao 1; Mgahawa 5; Wakala wa M-Pesa 15; Nusu Jumla 7; Nyumba ya kulala wageni 13; Pembejeo za Kilimo 1; Pharmacy 1; Vifaa vya Pikipiki 4; Stationery 5; Tiba asilia 2; Vifaa vya baiskeli 1; Vifaa vya Magari 1; Vifaa vya Mashine 1; Vifaa vya simu 1; Vifaa vya ujenzi 7; Vifaa vya Umeme 4; Wakala wa huduma za kifedha 4; Wakala wa NMB 1; Zahanati 1.